

## **Kujenga Mtandao Wako wa Ukereketwa**

Washiriki watajifunza jinsi ambavyo mitandao ya kijamii inaweza kutumiwa kuimarisha juhudi za utetezi. Washiriki pia watajifunza jinsi ya kuunda maudhui kwenye mitandao ili kusambaza maelezo kuhusu sababu ya kupendelea.

# **Kutumia Mitandao ya Kijamii ya Binadamu kwa Utetezi**

## **Sehemu ya Kwanza**

### **Ambia Wanafunzi Wako**

Kuna usemi maarufu unaosema, “haijalishi unafahamu nini. Cha mno ni nani unamfahamu.” Huenda kauli hii sio kweli 100% (kwa sababu unachofahamu pia ni muhimu sana!), ni makumbusho muhimu kuhusu umuhimu wa mitandao.

Iwe unatafuta kazi au unajaribu kushiriki kwenye michezo katika kiwango kingine, kukuwa na mtandao mzuri kunaweza kukupa fursa ya kupatana na watu wanaoweza kukusaidia ili ufikie malengo yako. Jitihada za utetezi huwa sawa pia. Kadri tunakuwa na mtandao mkubwa na mzuri wa watu tunaowafahamu, ndivyo inakuwa rahisi kwetu kuleta mabadaliko katika jamuiya zetu.

Kuanzia wanafamilia zetu na marafiki hadi walimu na viongozi katika jamuiya, tayari tunafahamu watu wengi wa kutosha, haswa tunapowajumuisha marafiki wa marafiki na tuendeleze mtandao wetu zaidi kando na wale waliokaribu nasi. Watu hawa wanaweza kuwa rasilimali muhimu sana katika azma yetu ya kufikia malengo yetu.

Kuna watu wengi ambao huenda bado hatuwafahamu ambao wanaweza kutusaidia kufikia malengo yetu. Mitandao ya kijamii na Intaneti hutoa njia nyingine pana zaidi ya kukutana na watu ambao huenda wanaweza kuchangia stadi na rasilimali katika jitihada zetu za utetezi.

## **Sehemu ya Pili**

Kwenye kiwambo kikubwa kilicho sehemu ya mbele chumbani, onyesha Ushawishi Uliofichwa wa Mitandao ya Kijamii au mfano wa video inayoambatana na muktadha wako / wa mtaani kwa mshiriki / wa kikanda ili uonyeshe jinsi watu walivyo unganishwa kupitia mitandao ya kijamii na jinsi tunavyoweza kunufaika kupitia miunganisho hii.

### **Uliza Wanafunzi Wako**

Je, habari zinaweza kusambazwa vipi kupitia mitandao yako ya kijamii iliyopo?

Je, tunaweza kutumia vipi miunganisho hii kuendeleza jitihada za utetezi?

### **Ambia Wanafunzi Wako**

Katika shughuli ifuatayo, utaandaa rasilimali ya mtandaoni inayoweza kushirikiwa ambayo hufafanua shughuli ambayo unafuatilia kwa dhati. Kwa kushiriki jitihada

zako za utetezi mtandaoni, unaweza kuwaambia watu wengine kuhusu shughuli unayofuatilia kwa dhati na ikiwezekana ukutane na watu wapya wanaoweza kukusaidia katika jitihada zako!

# Kazi

## Sehemu ya Kwanza

### Ambia Wanafunzi Wako

Andaa rasilimali ya mtandaoni inayoweza kushirikiwa (m.f., kwa kutumia Google Docs, jukwaa la mtandao wa kijamii, blogu ya Wordpress, tovuti kwenye Neocities, wasilisho kwenye slaidi kwa kutumia Scratch, n.k.) kuhusu jambo unalojali, ambapo:

1. Utaandika utangulizi ukieleza shughuli hii na sababu zinazokufanya uamini kwamba ni muhimu.
2. Weka viungo vya tovuti mbalimbali vinavyohusiana na jambo hilo (m.f., Makala yaliyo mtandaoni).
3. Orodhesha watu watatu wanaoandika maudhui kwenye blogu, tweet au kuunda maudhui ya kidijitali kuhusu shughuli hii. (Kwa hiari: Ikiwa unaweza, mwandikie kila mmoja wa watu hawa na uwaambie kuhusu shughuli yako na lengo lako unalotaka kufikia.)

### Mwingiliano wa Darasa

Wape washiriki dakika 30 kukamilisha shughuli hii. Kwa kutegemea muda uliotengwa, katika kikundi cha sasa au cha pili kinachokutana, waulize washiriki rasilimali zao kwenye kikundi kikubwa na wafanye mjadala wa dakika 15 huku wakiangazia mikakati ifaayo.